



**Mafunzo ya Biblia**

# **Yuda**

# Yuda

Yuda anawaandikia waamini kwa kuwahimiza wawe waaminifu kwa ukweli na kuzingatia mafunzo waliyopewa ma mitume wa Kristo. Amekua kutoka kwa familia ya Yesu nyumbani katika utoto wake, mpaka kuwa mtumwa mwaminifu wa ndugu yake, bwana wetu Yesu Kristo. Anaongea kwa uzito, kuhuzu vile Yesu alivyo na uwezo wa kutupandisha katika maisha haya hadi maisha ya uzima wa milele kwa ushindi mkuu.

## Uaminifu kwa Ukweli

Kunao miongoni mwetu wanao onekana kuwa waamini lakini hao sio. Wanafunza kuwa neema ya Mungu ni kwamba dhambi haijalishi kwa sababu Mungu atatusamehe, haswa, wanasema usinzi sio kitu kikubwa, kwa hivyo tunaweza kutimiza tamaa zetu na Mungu ataipuuza. Kilicho wazi kutokana na mafunzo yao ni tabia zao, ni kwamba wanamkana Kristo. Kama waaminio wa kweli, Kristo ndio kiini na kuitolewa kwetu wake lazima iwe kwa ukamilifu. Yuda anawakumbusha wasomi wae kwamba, ingawa wengi waliokolewa kutoka mizri, hawakuingia katika nchi ya ahadi kwa sababu ya kutokuwa waaminifu. Anaongea juu ya malaika waliofurahia mbinguni lakini walifungwa na minororo ya milele wakati walipoeda kinyume na maenzi ya Mungu na wao ukumu yao ya mwisho itatokea wakati Yesu aaporudi ena. Ni kitu cha kuofisha wakati watu wanapofurahi sana na dhambi zao, kwamba Mungu anachagua kuondoka na hawapati toba kamwe!

## Hukumu ya Moto wa Milele

Moto wa milele wa kuzimu ni ukweli mbaya sana kuelezea lakini Sodoma na Gomora ni mfano wa hatima ya wale wanaokataa maadili. Matumizi mabaya ya zawadi ya miili yetu, hufungua vita kubwa ya kiroho na ni wacha Mungu tu wanaoweza kutegemea uingiliaji wa Mungu wetu mwenye nguvu, kutuchukua salama kutoka duniani hadi mbinguni. Mapishano juu ya mwili wa Musa inaandikwa na ni picha ya vita kwa ukombozi kutoka kwa sheani ambao kila mmoja wetu anahitaji. Yuda anaelezea mitazamo kadhaa ya moyo wa mwanadamu, ambayo inaweza kutoa taswira ya utauwa lakini iko mbali na kile Mungu anataka.

## Njia ya Kaini

Matoleo ya Kaini alikataliwa kwa sababu aliamini wamba anaweza kumpendeza Mungu kupitia kwa juhudi zake. Balamu alikuwa nabii lakini hakuwa anatembea na Mungu. Kora alikuwa Mlawi lakini uasi uliingia moyoni mwake na hukumu ya Mungu ilikuwa kali sana - ardhi ilifunguka na kummeza yeye na familia yake! Dini na kazi nzuri haziwezi kutuokoa, ni kazi ya Kristo tu juu ya msalaba inaweza kuokoa. Kuwa na tamaa na ubinafsi bila kujali wengine, itavuna hukumu. Wachugaji ambao hawajitolei kwa kondoo lakini wanaona tu mahitai yao, watana ghadabu ya Mungu. Watu kama hao ni watupu, hawapati matunda, hawana mizizi, hawana malengo na wanaelekea umilele uliopotea!

## **Kutomcha Mungu**

Historia imeeleza wakati wa kutokuwa na uungu kiajabu, kama wakati wa Nuhu. Kwa kusikitisha, watu wanaobembelea, wanaolalamika, wakaidi, hao bado wapo. Enoka alitembea na Mungu wakati wa uovu mkubwa na akaonya juu ya hukumu kubwa, akiashiria wakati ambapo Yesu atarudi na watakatifu wote, kutawala na kuongoza na kuleta hukumu kwa ulimwengu. Walakini, nyakati za mwisho zitaona juhudi za wale wanaokosa Roho wa Mungu, kuunda mgawanyiko kati ya wacha Mungu. Wanatumia suluhisho za ulimwengu, ambazo husababisha machafuko, kuchanganyikiwa na kuvunjika moyo.

## **Kujenga Imani**

Yuda anatueleza tujienge katika imani yetu takatifu. Imani ya kweli hutokana na usikia nen la Mungu, kulijua neon la Mungu, kuelewa neon la Mungu na kutii neon la Mungu. Kuomba kulingana na Roho mtakatifu itatupa nguvu na kutuwezesha kusahimili siku ile mbaya. Lazima tuwe makini kwa mwongozo wa Roho ili tuweze kuomba kwa ujasiri, hata kama hatujui jinsi ya kuitikia kwa hali iwayo ile. Kutembea katika upendo wa Mungu ni ya muhimu. Kupenda kile Mungu anapenda na kuthamini kile Anachothamini, kutatuweka kwenye njia sahihi. Tuko safarini kwenda mbinguni kwa hivyo, tunapongojea wito huo, tunataka kuishi kwa usahihi sisi wenyewe lakini pia tuwahurumie wasafiri wenzetu. Tunahitaji kuangalia wengine na kwa unyenyekevu kutafuta kuwasaidia kumkaribia Mungu, kwa kuishi kwa haki na kwa kukataa maelewano yoyote na viwango vya ulimwengu huu!

## **Salama Ndani ya Yesu**

Tuko katika usalama wa kindani katika ulimwengu huu wa udanganyifu, kwa sababu tumejipeana wenyewe kwa Yesu, yule atakae tulinda kutokana na kuanguka. Anatamani kutuleta mbele ya Baba, bila mawaa na kwa shangwe kuu. Yesu ni Mungu kweli ambaye ni mwokozi wetu na Kristo Bwana wetu, kwake pekee, kuna utukufu, ukuu, nguvu na mamlaka, sasa n ahata milele. Amina.

## **Vipengele vya Kuzingatia:**

1. Kristo anataka kanisa safi. Tunafundisha kwa usahihi juu ya maswala kama vile uasherati na uzinzi?
2. Angalia Kaini na Kora. Ni wapi tunaona uasi wanamna huu utokea katika makanisa yetu na tunawezaje kuishughulikia?
3. Ni njia zipi ambazo Shetani hutumia, katika majaribio yake ya kudhoofisha na kuharibu kanisa la Yesu?
4. Unawezaje kuwahimiza watu ili waienge Imani yao?
5. Yuda anaueleza uzuri na ukuu wa Kristo ulivyo kwetu sisi. Ni kwa namna gani unaweza fanya hivyo kwa wale wanao tuzunguka?